TANZANIA HIGHER LEARNING INSTITUTIONS TRADE UNION
P.O. BOX **11727 DAR ES SALAAM**, Tanzania
Email: katibu@thtu.biz.tc,
Mobile: +255 755 576 224
Website: http://thtu.biz.tc

Kumb. Na:THTU/2009/C/130 07/07/09

**Toka:** Mwenyekiri Taifa THTU **Kwenda:** Viongozi na Wanachama wa THTU,

**YAH: MAELEZO JUU YA NEMBO YA CHAMA**

Tafadhali tafakari nembo mpya ya THTU ambayo tunataka ndiyo iwe nembo rasmi ya chama chetu.

Maumbo yaliyoko kwenye nembo ya THTU yana maana na tafsiri zifuatazo:

1. **Ngao mbili zilizolandana:** zinawakilisha wafanyakazi waendeshaji na wanataaluma waliomo kwenye taasisi zetu. Ngao inaashiria ulinzi/utetezi madhubuti wa maslahi ya wafanyakazi wetu
2. **Pembe Tatu ya rangi ya njano:** Inawakilisha utatu wa vyama vya wafanyakazi, vyama vya wanataaluma na mabaraza ya wafanyakazi mahala pa kazi. Pia pembe tatu inawakilisha majukumu makuu matatu ya chama hiki yaani kutetea na kulinda maslahi ya wafanyakazi, maslahi ya kitaasisi na maslahi ya kijamii katika taasisi za elimu ya juu. Rangi ya njano inaashiria kuwa majukumu hayo matatu na umoja wa vyombo hivyo vitatu mahala pa kazi ndio vinakipa chama cha THTU uwezo na thamani kubwa katika kuleta maendeleo ya nchi na taasisi zetu.
3. **Mviringo wa buluu:** Unawakilisha nafasi ya elimu katika kuleta maendeleo ya kijamii, yaani elimu ya kweli ni bahari isiyo na mipaka.

Rangi za chama zilizopo kwenye nembo hii zina maana na tafsiri zifuatazo:
1. **Rangi nyeusi:** Chama hiki ni chama kiongozi kwa mfanyakazi Mtanzania
2. **Rangi ya kijani:** Chama hiki kitatumia njia za amani kupata maslahi bora kwa wafanyakazi. Kitafanya juhudi kupata ridhaa kwa njia ya majadiliano yenye nguvu za hoja na hoja zenye nguvu.
3. **Rangi ya Bluu:** Kazi kubwa ya chama hiki ni kutetea na kulinda maslahi ya wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na kuleta mafanikio ya elimu nchini
4. **Rangi Nyekundu:** Chama hiki kitakuwa imara na makini katika kutetea maslahi ya wafanyakazi, taasisi na jamii katika taasisi za elimu ya juu.

Ni matumaini yetu kuwa nyote mtatoa mchango wenu wa dhati katika kukiimarisha na kukijengea uwezo wa kuleta mabadiliko yenye tija sio tu kwa wafanyakazi na taasisi za elimu ya juu bali pia kwa jamii nzima ya Watanzania hasa ukizingatia kuwa tumepewa dhamana ya kuwapokea waana wa Watanzania wenzetu na kuwageuza kuwa rasilmali watu bora kwa maendeleo ya Taifa letu.